

SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR



WIZARA YA AFYA

TAARIFA YA MRIPUKO WA UGONJWA WA SURUA

Ndugu Wananchi,

Wizara ya Afya imekuwa ikifuatilia taarifa za uwepo wa ugonjwa wa surua katika visiwa vya Unguja na Pemba kutokana na kutolewa kwa taarifa zinazoonesha kuwepo kwa washukiwa wa ugonjwa wa Surua na hivyo kupelekea kufuatilia visa hivi kwa karibu ikiwemo kufanya uchunguzi wa kitaalamu. Hadi sasa, tumepokea jumla ya visa 80 huku Unguja vikiwa 65 na Pemba 15 kutoka katika vituo vyetu vya Afya, hakuna kifo ambacho kimehusishwa na ugonjwa huu. Aidha, jumla ya sampuli 30 zilikusanywa na 3 kati ya hizi imethibitishwa kuwa na ugonjwa wa Surua katika Maabara yetu ya Taifa, Dar es salaam.

Surua ni mojawapo ya magonjwa ya kuambukiza ambayo husababishwa na virusi aina ya "Morbillivirus paramyxvirus" vinavyoenea kwa haraka kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa njia ya hewa au kugusa maji maji yatokanayo na mwenye maambukizi. Ugonjwa huu huambukizwa pale mtu aliepata maambukizo ya vimelea hivyo anapokohoa au kupiga chafya au kugusa sehemu ambazo zinatumiwa na watu wengine. Ugonjwa huu huathiri watu wa rika zote lakini **Watoto chini ya umri wa miaka 5, Mama wajawazito na watu wenye upungufu wa kinga mwilini** huathirika zaidi hata kupelekea vifo.

Ndugu Wananchi,


Dalili za ugonjwa huu ni pamoja Homa kali, kukohoa, Mafua na Macho kua mekundu. Aidha, ugonjwa huu huambatana na vipele/harara ambazo

hujitokeza katika paji la uso nyuma ya maskio na hata mwili mzima oamoja na kupatikana kwa vidonda katika mdomo au koo kuuma. Ugonjwa huu hauna tiba maalum bali hutibiwa kutokana na ishara na dalili zinazojitokeza kwa mgonjwa. Endapo, ugonjwa huu hautagundulika na kutibiwa mapema, athari katika Maskio kutoka usaha, Pneumonia (homa ino athiri mfumo wa mapafu), upofu wa macho na Homa ya uti wa mgongo inaweza kutokea na kupelekea kupoteza maisha.

Hivyo, Wizara ya Afya inawataka wale wote ambao watakuwa na dalili kama zilivyoainishwa, wafike katika vituo vya Afya kwa matibabu stahiki kwa haraka. Aidha, Wizara inawataka watumishi na wamiliki wa vituo vya Afya, kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kwa kuzingatia utekelezaji wa "Infection prevention and control" ili tuwakinge watumishi na wateja ambao tunawahudumia katika maeneo yetu. Vilevile, Wizara yangu inatoa rai kwa wananchi wote kunawa mikono na kuendelea kutumia barakoa ili tuwakinge wengine dhidi ya ugonjwa huu pamoja na kuhakikisha wazazi/walezi wanawapeleka watoto wao kupata na kukamilisha chanjo ya surua ili kumkinga mtoto dhidi ya ugonjwa huu.

Ndugu Wananchi,

Wizara itaendelea kufuatilia mripuko wa ugonjwa huu ikishirikiana na WHO pamoja na washirika wengine wa maendeleo ili kudhibiti kwa haraka. Aidha tutaendelea kutoa taarifa mara kwa mara ili kuelimisha umma kuhusu mripuko wa ugonjwa huu.



**MHE. NASSOR AHMED MAZRUI,
WAZIRI WA AFYA
09/08/2022**